**Journal of Kiswahili and Other African Languages**
Vol. 2 No. 1 (2024): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v2i1.548


# Viashiria vya Kujiua: Uchunguzi wa Mhusika Kazimoto katika Riwaya ya *Kichwamaji*

**Adria Fuluge**
*Chuo Kikuu Mzumbe, Tanzania*

**Uwasilishaji wa Makala**
*Pokelewa: 2024-01-12*
*Rekebishwa: 2024-05-02*
*Kubalika: 2024-05-18*
*Chapishwa: 2024-05-19*

***Maneno Muhimu***
Kujiua
Ubwege
Viashiria
Wahusika

**Jinsi ya Kurejelea Makala:**
Fuluge, A. (2024). Viashiria vya Kujiua: Uchunguzi wa Mhusika Kazimoto katika Riwaya ya *Kichwamaji*. *Journal of Kiswahili and Other African Languages,* 2(1), 41-50.

*Copyright © 2024*
CC BY NC SA

**Ikisiri**
Wahusika katika kazi za fasihi huumbwa kwa ustadi mkubwa kwa lengo la kubeba tafakuri na fikra za mtunzi kuhusu maisha ya jamii. Katika uumbaji huo, aghalabu, binadamu husawiriwa kama kiumbe anayeteseka na anayeishi katika ulimwengu usiomjali, aliyezungukwa na mateso na ubwege[1], na anayeshindwa kukabiliana vyema na uhalisia wake (Wamitila, 2002). Mambo hayo, ndiyo huweza kusababisha afanye maamuzi fulani kama vile kujiua. Hivi ndivyo anavyofanya Euphrase Kezilahabi katika riwaya ya *Kichwamaji* (1974) anapomuumba mhusika anayejiua. Hata hivyo, kwa kuwa kujiua huambatana na viashiria mbalimbali, makala haya yanajadili viashiria vya kujiua kwa mhusika mkuu katika riwaya teule tu. Riwaya hiyo imeteuliwa kwa sababu ina mawanda ya kutosha yaliyowezesha kupata data zilizolengwa katika makala haya. Pia, riwaya hiyo imeteuliwa kama sampuli ya kuwakilisha riwaya nyingine zenye viashiria vya kujiua. Misingi ya Nadharia ya Udhanaishi imetumika katika uchunguzi, uchanganuzi na uwasilishaji wa matokeo. Data zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa matini. Mjadala umebainisha kwamba katika riwaya ya *Kichwamaji* vipo viashiria vinne vya kujiua vilivyomkumba Kazimoto kabla ya kujiua kwake. Viashiria hivyo ni kukata tamaa, kujitenga kijamii, kuzungumzia masuala ya kujiua na mabadiliko ya tabia. Makala yanahitimisha kwamba jamii inahitaji kupewa elimu ya kutosha kuhusu kujiua kwa wahusika pamoja na viashiria vyake ili iweze kumtambua na kumsaidia mtu mwenye viashiria vya kujiua.

## Utangulizi

Matukio ya watu kujiua yamekuwa yakiripotiwa na kuongezeka kila siku duniani kote. TUKI (2014) inaeleza kuwa dhana ya 'kujiua' inatokana na kitenzi 'ua' chenye maana ya kuondoa uhai wa kitu au mtu. Hiki ni kitendo cha mtu kujisababishia kifo kwa kufanya kitu kinachoharibu na kupoteza uhai wake. Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO, 2018) na (BBCswahili.com 2022), kujiua ni janga

[1]Mtazamo wa kidhanaishi unaopinga kuwepo kwa maana na ufahamu katika maisha ya binadamu, kutokana na kukata tamaa na kukosa tumaini la kuishi. Kwa mujibu wa Esslin (2001), ubwege ni hali ya kukosa nia ya kufanya jambo fulani na kutengwa katika imani za kidini, tabia za kiungu na mizizi ya akili na mawazo ya mtu. Hii ina maana kwamba ubwege ni kitendo cha kudadisi hali ya binadamu ya kuendelea kuishi ilhali maisha hayana maana tena.

kubwa linalowaathiri watu wa mataifa mbalimbali duniani kote. Shirika hilo linabainisha kuwa watu laki nane (800,000) hadi milioni moja (1,000,000) kila mwaka, hujiua duniani kote, huku wengi wakifanya majaribio ya kujiua. Takwimu za shirika hilo zinaonesha kuwa nchi ya Sri Lanka ni kinara kwa watu wake kujiua ikiwa na 35.3%, ikifuatiwa na Lithuania 32.7%, na Guyana 29%. Hapa Afrika nchi inayoongoza ni Angola yenye 20.5%, ikifuatiwa na Afrika ya Kati 17.5%, na Eswatin 14.7%. Katika Afrika Mashariki, Tanzania inashika nafasi ya 4 ikiwa na 7% huku Rwanda ikiwa ni kinara kwa kuwa na 8.5%, ikifuatiwa na Burundi 8% na Uganda 7.1%. Aidha, WHO (2018) na BBCswahili.com, 2022) yanaeleza kuwa idadi ya watu wanaojiua Afrika ni kubwa zaidi duniani, ambapo takribani watu 11 katika kila watu 100,000 hujiua kila mwaka. Taarifa hiyo inafafanua zaidi kwamba hiki ni kiwango kikubwa zaidi ya kile cha wastani cha kimataifa ambacho ni watu 9 kwa kila watu 100,000. Kulingana na taarifa hiyo, jamii nyingi hazina elimu ya kutosha kuhusu viashiria vya kujiua. Hivyo, wito unaotolewa ni kuwa na juhudi za pamoja za kuzielimisha jamii zetu kuhusu tatizo la kujiua ikiwa ni pamoja na kubainisha viashiria vyake.

Sambamba na WHO na BBCswahili.com, wataalamu mbalimbali wakiwemo Williams (1970), Friedman (1973), Durkheim (1979), Neubeck (1986) na Glucksman na Kramer (2017) wamelishughulikia tatizo la kujiua kwa mwegamo wa kisosholojia, kisaikolojia na kiafya. Kwa mfano, Williams (1970), Friedman (1973), Durkheim (1979) na Neubeck (1986) wanaeleza kwamba watu wengi hujiua kwa sababu ya kukata tamaa ya kuishi, pamoja na kusongwa na matatizo ya kiakili. Pia, wanabainisha kuwa kujiua huchochewa na sababu mbalimbali, zikiwamo za kitabia, kijamii, kibaiolojia, na kiutamaduni; na kwamba, ni vigumu kumbainisha na kumtambua mtu anayepanga kujiua, kwa sababu anayejiua anajua kinachoendelea kichwani mwake. Wataalamu hawa wanabainisha sababu za mtu kujiua kuwa ni pamoja na sonona, maradhi ya hisia, na matumizi mabaya ya pombe na dawa za kulevya.

Tafiti nyingine zikiwamo za Freud (1900), Ndosi na wenzake (2004) na Glucksman na Kramer (2017) zinazoonesha kwamba kujiua ni tatizo la kisaikolojia linalohusishwa na masuala ya kiafya yanayoshambulia mfumo wa akili. Kwa mujibu wa Freud (1900) binadamu ana sehemu inayofahamika kama 'ung'amuzibwete' wa kibinafsi, ambapo fikra na mawazo mengi hasi hubuniwa na kuhifadhiwa. Anafafanua zaidi kuwa sehemu ya akili ya binadamu huhodhi fikra, mawazo, hofu na mitazamo hasi, ambayo haiwezi kukubalika katika jamii. Anahusisha masuala ya saikolojia na ndoto. Anaeleza kwamba ndoto huhusisha matukio yaliyotendeka zamani yanayobeba maana na ukweli kuhusu maisha. Anafafanua zaidi kwamba kupitia ndoto, mtu anaweza kukiuka miiko iliyowekwa na jamii na kujikamilishia utashi wake pasipo kukatizwa wala kukatazwa na wanajamii wengine. Hii ni kwa sababu anayeota ndoto, mara nyingine, huamini kwamba anayoota ni kweli. Hivyo, kitendo hicho huweza kumsababisha achukue uamuzi autakao kama vile kujiua kunakoambatana na viashiria mbalimbali.

Kwa mujibu wa Kubller-Rose (1991) viashiria ni ishara, dalili, au vitu vinavyoweza kutoa ufahamu au habari juu ya jambo fulani. Akifafanua kuhusu viashiria vya kujiua anasema kwamba hizi dalili au ishara zinazoweza kutokea mtu anapojaribu kujiua au anapokuwa katika hatari ya kufanya hivyo. Kimsingi, utafiti kuhusu viashiria vya kujiua unatakiwa kufanywa pia katika fasihi kutokana na ukubwa wa janga hili. Sababu kubwa ni kwamba elimu kuhusu viashiria vya kujiua na tatizo lenyewe la kujiua, bado haijatolewa kwa kina katika jamii zetu, ndiyo maana tatizo hili linaendelea kushamiri kila siku. Hivyo, kuna haja ya kuendelea kufanya tafiti katika nyuga mbalimbali ikiwemo fasihi ili kutoa elimu kuhusu janga lenyewe pamoja na viashiria vyake. Hii ni kwa sababu, fasihi ni sanaa ya lugha yenye ubunifu inayosawiri vipengele vya maisha, mahusiano, mazingira na hisia za watu katika muktadha fulani (Mulokozi, 2017). Pia, hutumika kama nyenzo ya mawasiliano na burudani

katika jamii, kwani hutoa mafunzo kuhusu tamaduni za jamii husika. Hivyo, kwa kuwa Tanzania pia inakumbwa na tatizo la watu kujiua na linazidi kushamiri, tumepata msukumo wa kuandika makala haya ili kubainisha viashiria vya kujiua kwa wahusika[2] kwa kurejelea riwayateule. Msukumo huu ulitokana na ukweli kwamba, licha ya tatizo hilo kushughulikiwa zaidi katika nyuga mbalimbali, bado linaendelea kushamiri katika jamii. Aidha, tafiti za fasihi ya Kiswahili hazijabainisha kwa uwazi viashiria vya kujiua kwa wahusika licha ya kuwepo kwa wahusika wanaojiua katika riwaya teule. Kutokana na hilo, tulipata hamasa ya kulishughulikia suala hili kwa mwegamo wa kifasihi kama njia mojawapo ya kutoa mchango wa uga huu katika jitihada za kuielimisha jamii kuhusu tatizo la kujiua. Kwa hiyo, makala haya yamechunguza viashiria vya kujiua kwa mhusika mkuu katika riwaya ya *Kichwamaji* (1974).

**Msingi wa Nadharia**
Utafiti uliozalisha makala haya uliongozwa na Nadharia ya Udhanaishi. Mtafiti aliongozwa na mihimili ya nadharia hii katika mchakato wa kukusanya data, kuzichambua na kuziwasilisha. Kwa mujibu wa Camus (1984) udhanaishi ni falsafa inayoshughulikia masuala mbalimbali kuhusu maisha. Anaugawa katika mitazamo miwili: mosi, maisha kama ombwe, yaani mahali patupu, na kwamba hayana maana yoyote. Pili, kujiua kama suluhisho la matatizo anayoyapitia binadamu duniani. Wamitila (2003) anasema udhanaishi ni mtazamo unaohusiana na hali na maisha ya binadamu, nafasi na majukumu yake ulimwenguni na uhusiano wake na Mungu. Anafafanua kwamba falsafa ya udhanaishi inatokana na mawazo ya Soren Kierkegaard (1813 – 1855) katika vitabu vyake vya *Fear and Trembling* (1843), *The Concept of Dread* (1844), na *Sickness unto Death* (1849). Kwa ujumla, wadhanaishi huyaona maisha ya mtu kuwa ni ya kitanzia na hayana maana, kwa kuwa mwisho wake ni kifo. Uchunguzi wa makala haya umejikita katika mihimili minne ya Udhanaishi. Mosi, kutafuta uhuru binafsi na uwezo wa mtu wa kujifikiria na kujiamulia mambo yake. Pili, kukengeuka misingi ya jamii. Tatu, kukata tamaa na mauti. Nne, kutoamini kuhusu uwepo wa Mungu. Mihimili hii imekuwa mwongozo katika kujadili viashiria vya kujiua kwa Kazimoto katika riwaya ya *Kichwamaji*. Viashiria hivyo vimejadiliwa kwa mwegamo wa kifasihi kwa sababu, fasihi huusawiri ulimwengu kulingana na maendeleo ya jamii na kuzifanya kazi za fasihi kufungamana na miktadha iliyozizaa kama asemavyo Fuluge (2021).

**Methodolojia**
Makala haya yametumia mkabala wa kitaamuli katika ukusanyaji, uchanganuzi, pamoja na utoaji wa matokeo. Uwasilishaji wa matokeo ulihusisha tafakuri binafsi, taarifa mbalimbali za kitafiti, nadharia husika pamoja na data za utafiti. Data hizo zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji na uchambuzi wa matini. Sampuli ya utafiti ilihusisha riwaya ya *Kichwamaji* (1974). Kadhalika, mtafiti alisoma maandiko mbalimbali yanayohusiana na mada yake ili kushadidia data za maktabani. Kwa kufanya hivyo, aliweza kubainisha viashiria vya kujiua kwa mhusika vinavyosawiriwa katika riwaya teule.

**Viashiria vya Kujiua katika Riwaya ya *Kichwamaji***
Sehemu hii inawasilisha matokeo ya utafiti kuhusu viashiria vya kujiua vilivyomkumba Kazimoto, kabla ya kujiua kwake. Utafiti umebaini viashiria vikuu vinne, ambavyo ni: kukata tamaa, kujitenga

[2] Wahusika katika bunilizi za kawaida ni binadamu, lakini viumbe wa aina nyingine au vitu visivyo na uhai huweza kutumika pia kutegemeana na fani yenyewe na lengo la mwandishi. Wahusika ndio watendaji wakuu; ndio kiini cha masimulizi, maana wao ndio huibua na kutengeneza mgogoro (Mulokozi, 2017).

kijamii, kuzungumzia masuala ya kujiua na mabadiliko ya tabia. Ithibati ya mjadala kuhusu vigezo hivi inatokana na hoja zilizomo katika riwaya ya *Kichwamaji* (1974).

**Kukata Tamaa**

Kiashiria kimojawapo cha kujiua ni kukata tamaa kunakotokana na mhusika kupitia changamoto mbalimbali katika maisha yake. Kukata tamaa, pia, ni sababu ya watu kujiua kwa kudhani kwamba wametengwa na jamii zao na dunia kwa jumla (WHO, 2022). Katika makala haya tumebainisha kuwa, mara nyingi mtu hufikia uamuzi wa kujiua kutokana na kuathirika kisaikolojia kiasi cha kukata tamaa na kuona kama dunia imemkataa na kwamba hawezi kuishi tena. Mtu huyo huamini kwamba, suluhisho lake ni kujiua. Suala hili linathibitishwa kupitia kwa Kazimoto baada ya kupitia changamoto mbalimbali katika maisha yake, ikiwemo ya kufiwa na mtoto wake. Viashiria vya kujiua kwake vinaanza kujitokeza baada ya kuwasili hospitalini na kuelezwa na Yaya namna mambo yalivyotokea. Anasema:

> Poleni sana Kazimoto, mtoto wako amerudi. Hakuweza kuishi. Wakati wa kujifungua ulipofika daktari alikuwa akifanya upasuaji kwa mtu mwingine. Mke wako alipata shida ya kuweza kupitisha kichwa cha mtoto ambacho kilikuwa kikubwa kupita kiasi. Daktari alichelewa kufika. Alipokuja mtoto alizaliwa lakini aliishi kwa muda wa saa moja tu (Kezilahabi, 1974: 179).

Katika dondoo hilo, Kazimoto anaumizwa na kukatishwa tamaa kutokana na maelezo ya Yaya kwamba sababu ya kifo cha mtoto wake ni kuchelewa kwa daktari wa kumhudumia mke wake. Maelezo hayo yanathibitisha kwamba licha ya mtoto huyo kuwa na kichwa kikubwa, huenda angepona kama daktari angefika kwa wakati. Maumivu yake yanazidi anapoingia katika chumba kimojawapo na kuwakuta Tuza na Sabina wanalia na kuzidisha maumivu yake kama anavyosema mwandishi kuwa:

> Nilikaa juu ya kitanda. Niliweka mkono wangu ndani ya mkono wa mke wangu ambaye sasa alilia kwa kwikwi. Sikuweza kusema neno lolote isipokuwa kusikitika kwa unyamavu (Kezilahabi, 1974: 179).

Kitendo cha Kazimoto kukaa kimya bila kusema jambo lolote kinadhihirisha namna alivyokuwa na maumivu makali kuhusu tukio hilo. Majonzi ya kufiwa na mtoto wake, yalimzamisha katika tafakuri kuhusu nafasi ya Mungu katika maisha yake. Anasema:

> Nilianza tena kufikiri juu ya Mungu. Kama kweli alikuwapo kwa nini aliweza kufanya ukatili mkubwa kama huo. Matumaini yetu yote; kazi na taabu tuliyopata – yote hayo chini! Sikuona maana ya kuishi (Kezilahabi, 1974: 180).

Kinachobainika katika dondoo hili ni kwamba Kazimoto anatafakari kuhusu nafasi ya Mungu katika mahangaiko yake. Kulingana na Nadharia ya Udhanaishi, Kazimoto anaonesha dalili ya kukata tamaa na kukana nafasi na uwepo wa Mungu kwa madai kwamba hamjali, ambapo hata ulimwengu wenyewe, nao, haumjali. Kauli yake kwamba haoni sababu ya kuendelea kuishi na kuzaa kizazi kibaya ni kiashiria cha kukata tamaa na kujiua kwake. Haya yanathibitika katika majadiliano yafuatayo baina yake na Sabina:

> "Mimi nimekata tamaa," nilimwambia mke wangu.
> "Tamaa ya nini?" aliniuliza kwa sauti yenye masikitiko mengi.
> "Ya kuishi – kupata watoto."
> "Mimi nina matumaini bado. Mungu ni mkubwa; Anafahamu kila kitu. Atatuwekea kitu kikubwa na kizuri zaidi. Anatujaribu kwa mateso ili kuona

> utulivu wetu. Bwana'ngu inafaa tuvumilie. Tukubali na tupokee lolote lile linaloporomoshwa na Mungu juu ya maisha yetu. Yeye ndiye anafahamu mabaya na mazuri."
> "Mimi siwezi kuishi tena," nilimwambia.
> "Kwa nini?"
> "Ulimwengu si pahala pa kuishi."
> "Unataka kwenda kuishi wapi?"
> "Ninataka kwenda kuishi mahali ambapo ninaweza kuishi bila kufikiri na bila kujua kwamba ninaishi" (Kezilahabi, 1974: 180).

Majadiliano haya yanaonesha namna Kazimoto na Sabina wanavyotofautiana kimtazamo kuhusu nafasi ya Mungu katika maisha yao. Wakati Kazimoto anaonesha kuwa maisha hayana maana na kwamba ulimwengu si mahali salama pa kuishi kama inaavyoelezwa katika Nadharia ya Udhanaishi, Sabina kwa upande wake anaweka matumaini yake kwa Mungu. Mtazamo wa Sabina unatofautiana na Kazimoto kwani haamini kuhusu uwepo wa Mungu, anayedaiwa kwamba ndiye muumba wa ulimwengu, ambao kimsingi kwake anaona kuwa haumjali. Utafiti unaonesha kuwa mjadala huo ni kiashiria cha kujiua kwa Kazimoto kutokana na kauli yake inayosema: "mimi siwezi kuishi tena." Makala yanabainisha kwamba, kwa wakati huu, Kazimoto yuko katika msongo wa mawazo unaotokana na tukio la kufiwa na mtoto wake. Katika mazingira hayo ni dhahiri kwamba anahitaji ushauri wa kisaikolojia ili kulikubali tatizo hilo. Kauli yake kwamba anataka kwenda mahali ambako hataweza hata kufikiri na kujua kama anaishi, ni dalili ya kukata tamaa na kiashiria cha kujiua kwake. Kwa mujibu wa makala haya, mtu akionesha kiashiria kama hicho, hatakiwi kuachwa peke yake kwa sababu kwa wakati huo anakuwa katika hatari ya kujiua. Pia, mtu wa namna hii hata akipata tatizo dogo tu, huamua kujiua kwa kudhani kwamba hana thamani katika jamii.

**Kujitenga Kijamii**

Hiki ni kiashiria kingine kinachoweza kusababisha mtu kujiua kutokana na upweke. Aghalabu, mtu huyo hujitenga na kuepuka mwingiliano na watu wengine na hupenda kubaki peke yake, huku akitafakari masuala mbalimbali yanayohusiana na maisha yake. Kwa msingi huo, mtu huyo akiachwa katika hali hiyo kwa muda mrefu, huweza kupata msongo wa mawazo, ambao humkatisha tamaa na hata kufikia hatua ya kuchukua maamuzi ya kujiua. Jambo hili linajitokeza kwa Kazimoto baada ya kubaini kwamba tabia yake ya umalaya, ndicho chanzo cha kifo cha mtoto wake. Kitendo hicho kinasababisha aanze kujitenga na mke wake na kukaa kimya muda wote wakiwa safarini na hata baada ya kuwasili nyumbani kwake. Anasema:

> Njiani sikuzungumza na Sabina maneno mengi. Kila mmoja alikuwa akiwaza yake. Tulipofika shuleni tuliomba ufunguo wa nyumba yetu kutoka kwa mwalimu aliyekuwa akitutunzia nyumba. Tulifungua na kuingia ndani kimya kama kwamba tulikuwa tukiingia kaburini. Nyumba ilionekana kuwa tofauti kabisa. Tulipoingia ndani tulikaa juu ya kochi, kupumzika kidogo. Tulikaa kimya (Kezilahabi, 1974: 194).

Nukuu hii ni ithibati kwamba mtu anapojitenga na jamii huweza kupata msongo wa mawazo, ambao kumsukuma katika kuchukua maamuzi fulani. Kwa mujibu wa Freud (1900), Ndosi na wenzake (2004) na Glucksman na Kramer (2017) msongo wa mawazo ni tatizo la kisaikolojia, ambalo humweka mhusika katika hali ya hofu kutokana na kuzidiwa na mawazo na kukosa jibu la kitu kilichoko mbele yake au kichwani mwake. Makala haya yanabainisha kwamba watu wengi hufikia uamuzi wa kujiua kwa sababu ya kukaa kimya na kuyakumbatia matatizo mbalimbali. Kujitenga kwa Kazimoto ni kiashiria cha kujiua kwake kwani kunamfanya asongwe na mawazo mengi kiasi cha kumfikirisha na

kumfanya ashindwe kuyatatua. Majadiliano baina yake na Sabina ni uthibitisho kwamba kujitenga kwake kunaashiria kujiua kutokana na kukata tamaa ya maisha. Haya yanathibitishwa kupitia nukuu ifuatayo:

> "Mke wangu," nilimwita.
> "Bwanangu," aliitikia.
> "Sijui kwa nini ninaishi."
> "Nimechoka na maswali yako ya kijinga," alisema.
> "Huwezi kuishi kama watu wengine?" Wewe nani?"
> "Mimi sijijui," nilimwambia.
> "Hakika sikufahamu kwamba wewe ni kichwamaji namna hii! Sikufahamu! (Kezilahabi, 1974: 194 - 195).

Katika nukuu hiyo, vinabainika viashiria vya wazi vya kujiua kwa Kazimoto. Majadiliano baina yake na Sabina yanaonesha kwamba amekata tamaa ya maisha na yuko tayari kuchukua uamuzi mgumu. Kwa mujibu wa makala haya, kukosekana kwa elimu ya saikolojia miongoni mwa watu tunaoishi nao, kunachangia katika kujiua kwa watu wenye viashiria hivyo. Tunathibitisha maelezo haya kupitia kwa Sabina ambaye kutokana na kukosa elimu hiyo, anashindwa kumsaidia Kazimoto katika matatizo yake. Badala yake anamwita Kichwamaji na kuamua kwenda kulala huku akimwacha katika upweke. Kitendo hicho kinazidisha tafakuri kwa Kazimoto kuhusu maana ya maisha. Anasema:

> Nilisimama pale dirishani kwa muda mrefu nikifikiri. Nilifikiri furaha; ilikuwa imetawaliwa sana na huzuni. Salima ambaye siku moja alitwambia kwamba kwa jambo lile alikuwa haoni tofauti yetu na ng'ombe, yeye mwenyewe hana raha sasa. Wakati nilipokuwa nikifikiri juu ya maisha nilisikia kitu fulani kama sauti ikiniita" "Kazimoto!" Sauti ilisikika polepole. "Naam," nilijibu kimoyomoyo. Nilikwenda ndani ya chumba cha kulala. Sabina alikuwa amejifunika shuka akilia kwa kwikwi. Nilichukua kitu fulani. Nilikuwa sifahamu jambo nililokuwa ninafanya, isipokuwa nguvu fulani zilikuwa zikiniongoza – sauti! Sauti! (Kezilahabi, 1974: 195).

Nukuu hiyo inaonesha namna Kazimoto alivyozama katika tafakuri nzito kuhusu maisha anayopitia. Makala haya yanaonesha kwamba mtu anayepanga kujiua wakati mwingine huwa na viashiria vya kujitenga na jamii yake tofauti na mazoea ya kila siku. Pia, husikia sauti ikimwita na kumhimiza ajiue na kwamba kama atachelewa, watu wengine watakuja na kumuua kabla ya kujiua kwake. Sauti ya namna hiyo ndiyo inayoashiria kujiua kwa Kazimoto, kwani anaamua kuchukua silaha pasipo kutambua kitendo anachokusudia kufanya. Matokeo yanaonesha kwamba kitendo cha Sabina kumwacha Kazimoto katika upweke kinatokana na kukosekana kwa elimu ya kisaikolojia ya namna ya kumsaidia mtu mwenye msongo wa mawazo. Kutokana na hilo, Sabina anakuwa mtu wa kwanza kushuhudia kichwa cha mumewe kikivuja damu baada ya kujipiga risasi huku akiacha ujumbe unaosema:

> Nimejiua. Siwezi kuendelea kuzaa kizazi kibaya. Pia sikuona tofauti kati yangu na mdudu au mnyama. Akili! Akili! Akili ni nini? Pia nikiwa duniani sikupata kukutana hata siku moja na mtu anayeamini kwamba kuna Mungu. Watu wanaoogopa kufa na kwenda motoni hao nimewaona, tena wengi sana. Mtu ye yote asilaumiwe kwa kifo changu. Mimi, kabla ya kufa, ninaungama mbele ya ulimwengu kwamba nilimwua mdogo wangu ingawa sikumgusa (Kezilahabi, 195).

Ujumbe huu ni uthibitisho kwamba mara nyingi kujiua huwa hakutokei ghafla, bali huambatana na viashiria mbalimbali vinavyohitaji elimu ya kisaikolojia ili kumtambua mhusika. Kitendo cha Sabina kuondoka na kumwacha mumewe akiwa katika tafakuri ya kina, kinawakilisha jamii pana kwamba haina elimu ya kutosha kuhusu viashiria vya kujiua. Mwandishi wa riwaya hii anathibitisha hili kupitia kwa Manase anaposema: "Wengi waliosikia juu ya kifo cha Kazimoto walistuka sana" (Kezilahabi, 1974:195). Hii inaashiria kwamba kujiua kwa Kazimoto kulichangiwa na mvurugiko wa akili unaotokana na kujitenga na jamii yake baada ya kupitia mambo mbalimbali katika maisha yake. Hivi ndivyo inavyoelezwa katika Nadharia ya Udhanaishi kwamba kujitenga kijamii ni kiashiria cha mtu kujiua kwani humfanya atafute uhuru binafsi na uwezo wake wa kujiamulia mambo yake mwenyewe ikiwa ni pamoja na kujiua.

**Kuzungumzia Masuala ya Kujiua**

Kiashiria kingine cha mtu kujiua ni kuzungumzia mara kwa mara masuala ya kifo au kujiua. Aghalabu, mtu huyo hupenda kuongelea masuala ya kujiua au kuua mtu mwingine akiwa peke yake au katika mazungumzo ya kawaida. Vilevile, huweza kuzungumzia kuhusu kutokuwa na furaha, matumaini, au hata kufanya vitisho vya moja kwa moja vya kujiua. Mtu wa namna hiyo hupenda kuzungumzia njia za kujiua na namna kifo chake kitakavyokuwa. Kubller-Rose (1991) anabainisha kuwa mtu anapoongelea mara kwa mara masuala ya kujiua au kuua watu wengine huwa ni kiashiria kimojawapo cha kujiua. Anafafanua kwamba mara nyingi mtu huyo huzungumzia suala hilo kama masihara huku akionesha kwamba anaweza kujidhuru au hapendi kuishi duniani. Hili linajitokeza kwa Kazimoto, ambaye, baada ya kifo cha dada yake, Rukia, na kile cha mama yake, anatumia muda mwingi kutafakari juu ya vifo hivyo na namna kifo chake kitakavyokuwa. Anasema:

> Usiku nilianza kufikiri juu ya kifo. Nilifikiri jinsi kifo changu kitakavyonijia – kwa ugonjwa, kwa ajali au kwa kukatwakatwa na wezi? Labda kwa uzee au kwa sumu! Huenda nikajiua mwenyewe! … Niliona kwamba adhabu kubwa ya mwanadamu ni maisha yenyewe. Nilimkumbuka mlevi mmoja niliyemkuta akipiga mti mweleka mpaka akaumia mwenyewe. Maisha ndiyo yaliyokuwa yakimsumbua, wala siyo pombe. Wakati huo usiku niliyaona maisha chanzo cha yote (Kezilahabi, 1974: 84).

Katika dondoo hili vipo viashiria vya wazi vya kujiua kwa Kazimoto kwani anatafakari kuhusu kifo chake na namna kitakavyomjia. Kwa mujibu wa Nadharia ya Udhanaishi, maisha ya mtu ni ya kitanzia na hayana maana, kwani mwisho wa mwanadamu ni kifo. Vilevile, nadharia hii inamwona binadamu kama kiumbe anayeteseka na kuishi katika ulimwengu usiomjali; aliyezungukwa na mateso na anayeshindwa kukabiliana vyema na ulimwengu huo. Masuala hayo ndiyo yanayomsumbua Kazimoto kutokana na changamoto mbalimbali anazopitia katika maisha yake. Kwa mtazamo wake, binadamu amepewa adhabu ya kuyatunza maisha yake. Hata hivyo, maisha yenyewe siyo mepesi, bali ni adhabu kubwa kuyatunza. Zaidi ya hayo, mwenye dhamana nayo, huweza kuyatwaa wakati wowote autakao. Anasema:

> Hii ni adhabu ambayo kila mwanadamu amepewa kutunza maisha yake. Maisha ambayo hayashibishwi wala kuridhishwa. Zaidi ya hayo mwenye nguvu anatunyang'anya wakati wote bila hata kutuarifu (Kezilahabi, 1974: 84).

Nukuu hiyo inaonesha viashiria vya wazi vya kujiua kwa Kazimoto kutokana na kukata tamaa huku akitafakari kuhusu namna ya kuikabili adhabu ya kuyatunza maisha yake. Anafikia hatua ya kusema kwamba "Mwisho wa mwanadamu utaletwa na mwanadamu mwenyewe" (Kezilahabi, 1974: 84 - 85).

Kauli hii inadhihirisha kwamba yuko katika kilele cha tafakuri kuhusu maisha yake kama inavyoelezwa katika Nadharia ya Udhanaishi kwamba, binadamu anapokumbwa na matatizo huweza kukata tamaa na hufikiria hata kujiua. Hivyo, nukuu hiyo inaonesha kwamba kuna viashiria vya kujiua kwa Kazimoto kutokana na namna anavyotafakari kuhusu suala la kifo. Matokeo yanaonesha kwamba mtu anayezungumzia mara kwa mara kuhusu kujiua hatakiwi kuachwa peke yake. Pia, jamii isimchukulie mtu huyo kimasihara kwani mara nyingi anapofikia hatua ya kuzungumza hivyo, huwa anakuwa amedhamiria kujiua. Kwa msingi huo, jamii inatakiwa kuelimishwa kuhusu viashiria vya kujiua ili iweze kumsaidia mhusika kabla ya kufikia uamuzi wa kujiua. Kufanya hivyo kutapunguza athari mbalimbali zitokanazo na mtu kujiua.

**Mabadiliko ya Tabia**

Hoja ya msingi katika sehemu hii ni kuthibitisha kwamba mabadiliko ya tabia ya mtu tofauti na ile iliyozoeleka ni kishiria kimojawapo cha kujiua. Mara nyingi, mabadiliko hayo huambatana na vitendo mbalimbali visivyo vya kawaida na visivyoendana na maisha yake ya kawaida ambavyo hufanywa na mhusika. Vitendo hivyo ni kama vile matumizi ya dawa za kulevya, unywaji wa pombe kupindukia, kufurahi au kuhuzunika kupita kiasi, kuongea kupitiliza, tabia ya ukimya, uvivu na kukosa usingizi. Makala haya yanathibitisha kwamba mabadiliko ya tabia ya mhusika wakati mwingine huambatana na mvurugiko wa akili yake. Hili linajitokeza katika riwaya ya *Kichwamaji* kupitia kwa Kazimoto ambaye baada ya kwenda kuomba kazi kwa Mkuu wa wilaya na kuikosa, anaamua kunywa pombe nyingi kama njia ya kuyasahau maumivu yake. Anasema:

> … Nilikunywa pombe yangu kimya. … Niliagiza chupa mbili za Tusker. … Walipofunga baa nilinunua chupa moja ya Grenado. … Nilianza kunywa pombe nyingi ili nilewe upesi nisahau mambo. Chupa ilikuwa bado kwisha mawazo haya yalipopotea (uk. 14).

Kitendo cha Kazimoto kunywa pombe nyingi kwa madai kwamba anataka kusahau mambo mengi aliyonayo, ni kiashiria cha mabadiliko ya tabia yake. Kwa mujibu wa makala haya, kujiua ni jambo linaloelekeana sana na matendo yanayofanywa na mhusika kabla ya kitendo chenyewe cha kujiua. Mtu huyo huonesha hisia, fikra na tabia zisizokuwa za kawaida. Haya ndiyo yanayoshuhudiwa kwa Kazimoto kwani anapanga kumdhuru Mkuu wa Wilaya kwa sababu ya kumnyimwa kazi. Anasema:

> Wazo la kufika tu ofisini nimchome Manase visu vya tumboni lilinijia tena kichwani. “Huenda nami nikanyongwa,” nilisema moyoni. “Sitapata faida yoyote isipokuwa kuwaacha wazazi wangu taabuni. Jambo la maana ni kujaribu kumpa Manase maisha magumu hapa duniani. Nisipoweza basi nitajilipiza kisasi kwa njia nyingine (Kezilahabi, 15).

Kinachojitokeza katika dondoo hili ni kwamba Kazimoto anaonesha mabadiliko ya tabia kutokana na matatizo aliyonayo. Kitendo cha kupanga kwenda kumchoma visu Mkuu wa Wilaya kinaonesha kwamba amekata tamaa na haoni tena thamani ya maisha yake. Msimamo wa makala haya ni kwamba kubadilika kwa tabia ya Kazimoto kama inavyoelezwa katika Nadharia ya Udhanaishi kwamba binadamu hutafuta uhuru wake binafsi na uwezo wa kujifikiria na kujiamulia mambo yake mwenyewe, ni kiashiria cha kujiua kwake. Ni dhahiri kwamba kama kitendo cha kumuua Mkuu wa Wilaya kingefanikiwa, huo ungekuwa mwisho wa maisha yake ama kwa kujiua mwenyewe au kwa kuuawa na nguvu ya umma. Matokeo yanaonesha kwamba kitendo cha Kazimoto kunyimwa kazi, kinajenga chuki na visasi moyoni mwake na kinaashiria kujiua kwake.

Makala haya pia, yanabainisha kuwapo kwa mabadiliko ya tabia ya Kazimoto ya kupinga kuhusu uwepo wa Mungu, ambapo mtazamo wake unakinzana na mawazo ya wazee wanaoamini kuhusu

nafasi ya Mungu katika maisha yao. Kitendo cha Kazimoto kupingana nao, kinaonesha kwamba amekata tamaa ya maisha kutokana na mabadiliko ya tabia yake. Mtazamo wa wazee hao ni kwamba, Kazimoto amechanganyikiwa kama anavyosema mzee mmojawapo kwamba huyo ni mwehu:

> Mnazungumza na mwehu!" Alisema kwa kelele. "A! Anasema kwamba hakuna Mungu. Hakuna Mungu! Mtoto wa nani? Mababu na mababu wamekwenda; wamechukuliwa na nani? Bangi! (Kezilahabi, 1974: 51).

Katika nukuu hiyo, vipo viashiria vya mabadiliko ya tabia ya Kazimoto ya kukana kuhusu nafasi ya Mungu. Kwa kuzingatia Nadharia ya Udhanaishi, kupitia msingi unaopinga kuhusu nafasi ya Mungu, ni dhahiri kwamba, kitendo cha Kazimoto kudai kwamba hakuna Mungu kinaashiria kwamba amebadilika kitabia na anaweza kuchukua uamuzi wowote, hata wa kujiua, kama waaminivyo wadhanaishi. Ndiyo maana katika majadiliano yake na Manase anafikia hatua ya kusema kwamba wanaoamini kuhusu Mungu ni waoga.

> Unaona, Manase; mwanadamu ameamua kwamba kuna Mungu kwa sababu ya hali yake ya woga iletwayo na milango ya fahamu. Kwa hiyo mtu anayeamini kwamba Mungu yupo ni yule aamuaye kwa kufuata milango ya fahamu zake. Kwake fahamu zinatawala bongo (Kezilahabi, 1974: 124 - 125).

Kinachothibitika katika nukuu hiyo ni mvurugiko wa akili ya Kazimoto kutokana na changamoto mbalimbali anazopitia katika maisha yake. Changamoto hizo zinamfanya abadilike kitabia na kukengeuka kaida za maisha ya jamii yake za kuamini kuhusu nafasi ya Mungu. Kitendo cha kufiwa na mtoto wake kinampa msukumo zaidi wa kutafakari juu ya Mungu. Anasema:

> Nilianza tena kufikiri juu ya Mungu. Kama kweli alikuwapo sikuona kwa nini aliweza kufanya ukatili mkubwa kama huo. Matumaini yetu yote; kazi na taabu tuliyopata yote hayo chini! Sikuona maana ya maisha (uk. 180).

Dondoo hilo linaonesha namna Kazimoto alivyofika katika ukingo wa fikra na tafakuri yake kuhusu Mungu. Haoni tena nafasi ya Mungu katika maisha yake kama inavyoelezwa katika Nadharia ya Udhanaishi kwamba mtu mwenye viashiria vya kujiua hufikia hatua ya kuona kwamba hakuna Mungu. Hii ni kutokana na matatizo mbalimbali yanayomkumba katika maisha yake kama inavyomtokea Kazimoto. Kimsingi, hiki ni kiashiria cha kujiua kwake kwani anadai kwamba haoni tena maana ya kuishi na wala haoni sababu ya kuamini kuhusu Mungu. Kwake, uwepo wa Mungu hauna maana kwa sababu hajamsaidia kutatua matatizo yake.

## Hitimisho

Makala haya yamebainisha viashiria vya kujiua kwa mhusika katika riwaya ya *Kichwamaji*. Makala yamethibitisha kwamba kujiua ni janga linalozikumba jamii zote duniani kote. Mjadala umeonesha kuwa kabla ya kufikia kitendo chenyewe cha kujiua, mhusika huwa na viashiria fulani visivyoendana na tabia yake ya kawaida. Viashiria vinne, ambavyo ni kukata tamaa, kujitenga kijamii, kuzungumzia masuala ya kifo, na mabadiliko ya tabia vimejadiliwa. Viashiria hivyo vimebainika kutokana na uchambuzi wa riwaya ya *Kichwamaji* (1974) kwa kumhusisha mhusika mkuu, Kazimoto. Imebainika kwamba mhusika huyu baada ya kupitia changamoto mbalimbali katika maisha yake, hatimaye, aliamua kujiua. Aidha, imedhihirika kwamba ijapokuwa mhusika alionesha vishiria mbalimbali kabla ya kujiua kwake, jamii ilishindwa kumsaidia kutokana na kukosekana kwa elimu ya namna ya kumtambua mtu mwenye viashiria vya kujiua. Hivyo, jamii inatakiwa kuelimishwa kuhusu masuala ya kujiua na kupewe elimu kuhusu afya ya akili. Vilevile, ielimishwe namna ya kumtambua mtu

mwenye viashiria vya kujiua ili iweze kumsaidia anapohisi viashiria vya kujiua kwake. Hii itapunguza idadi ya vifo vinavyotokana na watu kujiua.

**Marejeleo**

BBCswahili.com (2022). Dira ya Dunia. Taarifa ya Habari za Dunia. Siku ya Alhamisi tarehe 10.9.2022 saa Tatu Usiku.
Camus, A. (1984). *The Myth of Sisyphus, and Other Essays.* Penguin.
Durkheim, E. (1979). *Suicide: A Study in Sociology* (Translated by J. A. Spaulding & G. Simpson). The Free Press. (Original Work Published in 1897).
Esslin, M. (2001). *The Theatre of the Absurd*. Vintage Books.
Fuluge, A. (2021). *Usawiri wa Mchakato wa Kujiua katika Riwaya za Euphrase Kezilahabi: Ni Mwangwi wa Mtanziko wa Kijamii?* Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.
Freud, S. (1900). *"The Interpretation of Dreams. The Complete and Definitive Text"*, Translated and Edited by James Strachey (2010). Basic Book Group. The Hogarth Press Limited.
Friedman, M. (1973). *Burried Alive: The Biography of Janis Joplin*. Harmony Books.
Glucksman, M. L., & Kramer, M. (2017). "Manifest Dream Content as Predictor of Suicidality. *Psychodynamic Psychiatry", 54(2)*, 175 - 185.
Kezilahabi, E. (1974). *Kichwamaji*. East Africa Publishing House.
Kubler-Ross, E. (1991). *On Death and Dying*. Macmillan Publishing Co.
Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. KAUTTU, Limited.
Ndosi, N. K., Mbonde, M. P., & Lyamuya, E. (2004). "Profile of Suicide in Dar es Salaam". *East African Medical Journal*, 81(4), 207 - 211.
Neubeck, K. (1986) *Social Problems: A Critical Perspective*. Random House.
TUKI. (2014). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Oxford University Press.
WHO. (2018). Tanzania ya 27 Afrika Matukio ya Watu Kujinyonga: (*Mtanzania*, 25 Januari, 2018; uk.1, 4).
WHO. (2022). Idadi ya Wanaojiua Afrika ni Kubwa Zaidi Duniani; WHO Yazindua Kampeni Kuzuia Tatizo Hilo. Inapatikana katika https://news.un.org, 2022/10. Ilipakuliwa tarehe 20 Disemba, 2023.
Williams, R. M. (1970). *American Society: A Sociological Interpretation*. Random House.
Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele Vyake*. Phoenix Publishers Limited.
Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Focus Books Publications Limited.